# MILAMBO CO - OPERATIVE UNION LIMITED

**MILAMBO CU (2018) LTD - REG. NO AFF-TBR-URA-DC-2023-57**

Telegraph: 'MILAMBO'
Tel:
Mob: 255765-567-584
Fax:
E-Mail:
*milambocultd@gmail.com*

**Bomani Road,**
P.O. Box 186,
URAMBO.

**Kumb Na.AC7/199/01/41.** 15 SEPTEMBA, 2026.

## TANGAZO LA ZABUNI YA UJENZI.

### 1.0 UTANGULIZI

**Milambo Co-operative Union Limited (2018) Ltd** ilianzishwa mwaka 2018 kufuatia kujitenga na Chama Kikuu cha Ushirika WETCU. Makao makuu ya chama yapo katika Wilaya ya Urambo, Chama kimesajiliwa rasmi kwa usajili namba **MILAMBO CU (2018) LTD-REG.NO AFF-TBR-URA-DC-2023-57.**

Katika kuendeleza mipango yake ya maendeleo na kuimarisha huduma kwa wanachama wake, **Milambo Co-operative Union Ltd (2018)** inaendelea kutekeleza **mradi wa ujenzi wa jengo la biashara (MILAMBO COMMERCIAL COMPLEX) na ukumbi wa mikutano(FLEXIBLE HALL)** katika wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora.

Utekelezaji wa mradi huu tayari unaendelea na unafanyika kwa utaratibu wa **FORCE ACCOUNT**. Hivyo, wananchi wote wenye sifa, uzoefu na uwezo katika hatua/kazi zifuatazo wanakaribishwa kutuma maombi yao ili kushiriki katika utekelezaji wa kazi za mradi huu.

I. **Upauaji wa Majengo kwa kenchi za chuma na bati.**
II. **Uwekaji wa dari (Supply and fix Vinly suspended ceiling tiles)**
III. **Uwekaji wa sakafu aina ya terazo (Supply and fix)**
IV. **Upigaji lipu na Uwekaji wa vigae vya ukutani.**
V. **Skimming,Upakaji wa rangi na Mapambo.**
VI. **Utengenezaji na ufitishaji wa milango ya mbao ngumu na milango ya aluminium(Supply and fix)**
VII. **Utengenezaji na ufitishaji wa madirisha ya chuma na ya Aluminium (Supply and fix).**

**2.0 SIFA ZA MUOMBAJI:**

i. Awe na uwezo wa kusoma ramani na kuitafsiri vizuri.
ii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi na taasisi za umma au binafsi (nyaraka za uzoefu katika kazi husika ziambatanishwe)
iii. Awe na mafundi wasaidizi wakutosha wenye uwezo mzuri na awe na uwezo wa kuwasimamia.
iv. Awe na mtaji wa kuanzia kwani hakutakuwa na malipo ya awali bali atalipwa kulingana na gharama ya kazi itakayokuwa imefanyika na kukubaliwa na mhandisi wa ujenzi.
v. Awe mwaminifu na mwadilifu.
vi. Awe na TIN namba na akaunti namba ya benki.
vii. Awe na mashine ya risiti ya kielektroniki (EFD MACHINE) kwa kazi ambazo anajitegemea vifaa(supply and fix).

**3.0 MASHARTI YA KUTUMA MAOMBI:**

i. Muombaji anatakiwa kufika na kuona sehemu na mazingira ambapo kazi hizo zitafanyika kwa kuona Majengo na kupewa maelekezo ya kitaalamu itakapohitajika.
ii. Kabrasha za zabuni zinapatikana Ofisi ya Milambo Union kuanzia saa 2:00(mbili kamili) asubuhi hadi saa 10:00 (kumi kamili) alasiri.
iii. Muombaji aonyeshe gharama zake kwa kujaza kabrasha la zabuni na kurudisha likiwa limefungwa.
iv. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 25/09/2026 saa 6:00 (sita kamili) mchana na ufunguzi utafanyika mara baada ya kufunga zoezi hilo katika ofisi za Chama Kikuu cha Ushirika Milambo.
v. Waombaji/wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi huo.
vi. Maombi yawasilishwe kwa barua pepe au katika ofisi ya Chama Kikuu cha Ushirika Milambo iliyopo barabara ya Kigoma yakiwa katika bahasha iliyo fungwa vizuri kupitia anuani tajwa hapo chini.

**Meneja Mkuu,**
**Chama Kikuu cha Ushirika Milambo**
**S.L.P 186,**

**Tabora-Urambo**
*Barua pepe: milambocultd@gmail.com*

vii. Muombaji aonyeshe muda na mpango kazi atakaotumia kufanya na kukamilisha kazi hiyo.

viii. Ada ya Maombi ni Shillingi **Elfu Hamsini tu (Tsh 50,000/=)** za Kitanzania, ambayo itatolewa wakati wa kuchukua kablasha kama gharama za ununuzi na haitorudishwa.

**NB**:

- Maelezo ya kina ya kazi yanapatikana kupitia michoro na nyaraka za zabuni.
- Muombaji anaruhusiwa kuomba na kulipia kazi zaidi ya moja kwa kuambatanisha nyaraka za uzoefu wa kila kazi aliyoomba.

***Kwa mawasiliano zaidi piga +255756319641/0717523644***

Malipo yote yafanyike kupitia Akaunti za Benki (fedha taslimu (cash) hazitapokelewa)

**MILAMBO CU.LTD**
NMB – 51310019476
CRDB – 0150374252600

"Pamoja na Salamu za Ushirika"

.....................................
Innocent J. Tibesigwa
**MENEJA MKUU.**

MILAMBO CO-OPERATIVE UNION LIMITED
REG No. AFF-TBR-URA-DC-2023-057
P. O. Box 186
URAMBO